Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU NA LIBERATUS MWANG'OMBE**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI Na. 041/2020**

**HUKUMU KUHUSU MAMLAKA YA KISHERIA NA UKUBALIFU**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**ARUSHA, 6 Machi 2026**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama), leo imetoa hukumu katika kesi ya *Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Liberatus Mwang'ombe dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Maombi haya yamewasilishwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Liberatus Mwang'ombe. Mleta Maombi wa Kwanza na wa Pili wote wanarejelewa kwa pamoja kama "Waleta Maombi".

Mleta Maombi wa Kwanza ni shirika huru, lisiloegemea upande wowote na lisilo tengeneza faida la haki za binadamu ambalo lilipewa hadhi ya mwangalizi na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mleta Maombi wa Pili ni raia wa Tanzania, na ni mtetezi wa haki za binadamu. Waleta Maombi walidai kuwepo ukiukaji wa haki ya kujiandikisha na kupiga kura kwa maelfu ya mahabusu na raia wanaoishi ughaibuni, katika uchaguzi wa rais na bunge la kitaifa.

Waleta Maombi walidai kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi) ilikiuka Kifungu cha 1, 2, 3 na 13(1) vya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba), Kifungu cha 2(1), 2(2), 7, 25(a) na (b) vya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR), na Kifungu cha 2, 21(1) vya Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR), pamoja na Kifungu cha 13(2) na (4) vya Katiba ya Tanzania.

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510



Kwa umahususi, Waleta Maombi walidai kwamba Mjibu Maombi amekiuka haki za mahabusu, wafungwa na raia wanaoishi nje ya nchi kushiriki katika shughuli za serikali kupitia Kifungu cha 5(2)(c) cha Katiba yake, Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa (hapa inarejelewa kama "NEA"), na kushindwa kutoa kwa uthibitisho njia zinazowawezesha raia wanaoishi nje ya nchi kupiga kura.

Katika kuangalia mamlaka yake ya kisheria, Mahakama ilibainisha kwamba Mjibu Maombi aliibua pingamizi kuhusu mamlaka yake ya kisheria. Mjibu Maombi, kwanza alidai kwamba ukiukaji unaodaiwa kufanywa uko ndani ya mamlaka ya mahakama za kitaifa; na, pili, kwamba Mahakama inaombwa kufanya kazi kama mahakama ya mwanzo ikizingatiwa kwamba Waleta Maombi hawakuwa wamefika kwenye mahakama za ndani. Waleta Maombi kwa upande wao wanawasilisha kwamba Mahakama haiwezi kudaiwa kuwa inafanya kazi kama mahakama ya mwanzo kwa kushughulikia Maombi haya, kwa kuwa Maombi haya yanahusisha madai ya ukiukaji wa haki zinazolindwa na mikataba ambayo Mjibu Maombi ni mhusika.

Kuhusu pingamizi kwamba haina mamlaka ya kisheria kwa sababu ukiukaji unaodaiwa kufanywa uko ndani ya mamlaka ya mahakama za kitaifa, Mahakama ilirejelea maamuzi yake ya awali kwamba haizuiliwi kutumia mamlaka ya kisheria kwa sababu maswala yaliyowasilishwa mbele yake yalikuwa yameamuliwa katika mahakama za ndani. Kwa hivyo Mahakama iliona kwamba ina mamlaka ya kisheria maadamu inaombwa kuamua endapo kesi za ndani ziliendeshwa kulingana na viwango vilivyowekwa katika Mkataba na hati zingine za haki za binadamu zilizoidhinishwa na Mjibu Maombi. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi kwamba Maombi haya yanahusiana na masuala ambayo yako ndani ya mamlaka ya mahakama za kitaifa.

Kisha Mahakama iliangalia sehemu ya pili ya pingamizi kuhusu mamlaka yake ya kisheria kwa msingi kwamba iliombwa kufanya kazi kama mahakama ya mwanzo kwa kushughulikia madai yaliyotolewa kuhusiana na madai ya marufuku dhidi ya wafungwa, mahabusu (watuhumiwa) na raia wanaoishi katika nchi za nje wasipige

kura. Katika suala hili, Mahakama ilirejelea busara yake ya kisheria kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 3(1) cha Itifaki, ilikuwa na mamlaka ya kisheria ya kushughulikia maombi yaliyowasilishwa mbele yake, endapo tu madai ya ukiukaji wa haki zilizohakikishwa katika Mkataba au hati zingine zozote za haki za binadamu zilizoidhinishwa na Mjibu Maombi.

Ikirejelea katika kesi hii, Waleta Maombi walidai kufanyika ukiukaji wa haki zinazolindwa chini ya vifungu vilivyotajwa hapo awali vya Mkataba, ICCPR na UDHR, ambavyo Mjibu Shauri ni mhusika, Mahakama iliona kuwa haiwezi kuchukuliwa kuwa itakuwa ikifanya kazi kama mahakama ya mwanzo kwa kushughulikia Maombi haya. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pia sehemu hii ya pili ya pingamizi.

Kwa kuzingatia yaliyotajwa hapo juu, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi na ikasisitiza kuwa ina mamlaka ya kusikiliza Maombi haya.

Kuhusu vipengele vingine vya mamlaka, Mahakama ilibaini kwamba ilikuwa na mamlaka binafsi kwani Maombi hayo yaliwasilishwa kabla halijaanza kutumika ondoleo la Azimio la Mjibu Maombi chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki). Pia iliona kuwa ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulikuwa wa hali ya kuendelea, na mamlaka ya kieneo kwani ukiukaji huo ulitokea ndani ya eneo la Mjibu Maombi. Kutokana na yale iliyoyabaini kuhusu vipengele vyote vya mamlaka yake, Mahakama kwa kauli moja, ilitangaza kwamba ina mamlaka ya kusikiliza Maombi haya.

Kuhusu ukubalifu, Mjibu Maombi alidai kwamba marufuku inayodaiwa kuhusisha haki za wafungwa na mahabusu kupiga kura hapo awali ilikuwa imeshughulikiwa na mahakama ya ndani. Aidha alidali kwamba madai kama hayo yalikuwa yamesikilizwa na Mahakama yake Kuu katika kesi ya masilahi ya umma ya *Tito Elia Magoti na Mwingine dhidi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Wengine 2,* ambapo mahakama hiyo ilitangaza vifungu vya Ibara ya 11(1)(c) ya Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa kuwa

vipo kinyume cha katiba na ni batili. Anasema kwamba, katika kesi iliyotajwa, rufaa inasubiriwa mbele ya Mahakama ya Rufaa ambayo Waleta Maombi katika Maombi haya wanalazimika kusubiri matokeo yake ili kutimiza matakwa ya kukamilisha taratibu za ndani.

Kwa upande wao, Waleta Maombi walidai kwamba hawakuweza kukamilisha taratibu za ndani, kwani Kifungu cha 74(12) cha Katiba ya Mjibu Maombi kinamzuia mtu yeyote kupinga vitendo vya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (hapa inarejelewa kama "NEC"). Waliendelea kusema kwamba Kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu [Ibara ya 3 Toleo la 2019] (hapa inarejelewa kama "BRADEA"), kinazuia wale ambao hawajaathiriwa moja kwa moja na uvunjaji wa masharti ya Kifungu cha 12 hadi 29 vya Katiba kupinga vifungu hivi katika mahakama za ndani. Kwa hivyo ilikuwa hoja ya Waleta Maombi kwamba, kwa kuwa Maombi yao mbele ya Mahakama ya Afrika yalikuwa ni ya maslahi ya umma, hawakuweza kukamilisha taratibu za ndani.

Katika kushughulikia mapingamizi ya Mjibu Maombi kuhusu ukubalifu wa Maombi kulingana na kutokamilisha taratibu za ndani, Mahakama ilirejelea uamuzi wake wa awali kwamba sharti ni kukamilisha taratibu za kawaida za mahakama ambazo zinatoa matarajio ya mafanikio; ambayo pia yanapaswa kuwepo, yenye ufanisi, toshelevu, na yasiyotumia muda mrefu.

Katika kutumia kanuni hizi kwenye Maombi, Mahakama ilishughulikia taratibu mbili za ndani ambazo Waleta Maombi wanaweza kutumia, yaani: i) kupinga uhalali wa kikatiba wa Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa; na ii) kupinga vizuizi vinavyodaiwa kuwepo chini ya BRADEA.

Kuhusu kupinga uhalali wa kikatiba wa Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa, Mahakama iliangalia kesi ya *Magoti* ambayo Mjibu Maombi aliitumia kuweka hoja zake ambapo Mahakama yake Kuu iliamua kuhusu vizuizi vya kupiga kura vilivyowekwa kwa mahabusu wanaosubiri kesi zao kusikilizwa na wafungwa, masuala ambayo pia

yanajitokeza katika Maombi haya. Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi wote katika Maombi haya walikuwa na msimamo wa kupinga uhalali wa kikatiba wa Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa ikizingatiwa kwamba Kifungu cha 26(2) cha Katiba ya Mjibu Maombi, kinampa "mtu yeyote" uwezo wa kulinda Katiba na sheria za nchi. Kwa hivyo Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi hawakukamilisha utaratibu wa kupinga uhalali wa kikatiba wa Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa; na ilikubali pingamizi la Mjibu Maombi katika suala hili.

Kuhusu kupinga vizuizi vinavyodaiwa kuwepo kwa mujibu wa BRADEA, Mahakama ilitofautisha Maombi haya na yale yaliyoamuliwa katika maamuzi yake ya awali, ambapo iliona kwamba ombi la kikatiba kupitia BRADEA ni njia ya suluhu isiyo ya kawaida. Jambo tofauti ambalo Mahakama iliona ni kwamba maamuzi yake ya awali yalihusisha kesi za jinai za ndani zilizohukumiwa hapo awali na mahakama ya juu zaidi ya Mjibu Maombi. Katika hali hizo, Mahakama ilirejelea kwamba haikuwa busara kuwataka Waleta Maombi walewale kuwasilisha maombi mapya kuhusu ukiukaji wa haki zao za binadamu mbele ya mahakama ya chini. Kinyume na hali hizo, Mahakama iliona kwamba kutafuta suluhu kwa njia ya maombi ya kikatiba chini ya BRADEA haiwezi kuchukuliwa kuwa ni njia ya kutafuta suluhu isiyo ya kawaida; na badala yake ni njia ya kawaida ya kutafuta suluhu.

Baada ya kuona hivyo, Mahakama iliamua kuangalia endapo Waleta Maombi katika Maombi haya walikuwa na haki ya kuwasilisha ombi kwa mujibu wa BRADEA. Mahakama ilirejelea uamuzi wake wa wali katika kesi ya *Kituo cha Haki za Binadamu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*, ambapo iliona kwamba taratibu za ndani hazipaswi kukamilishwa katika hali ambapo mashirika yasiyo ya kiserikali yanayowakilisha maslahi ya watu binafsi yanazuiwa kuzifikia mahakama za ndani za Mjibu Maombi, kwani taratibu za ndani zinachukuliwa kuwa hazipo. Mahakama pia ilirejelea uamuzi wake katika kesi hiyo hiyo kwamba katika mfumo wa ndani wa Mjibu Maombi, mtu yeyote ambaye hakuweza kuonyesha kuwa mwathiriwa alizuiwa kutekeleza ombi hilo kwa mujibu wa BRADEA.

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510



Katika kutumia mfano huu kwenye Maombi haya, Mahakama ilibainisha kwamba Waleta Maombi hawakuwa na haki ya kuwasilisha ombi kwa mujibu wa BRADEA. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba njia hii ya kupata suluhu haikuwepo na inapaswa kuchukuliwa kuwa utaratibuu huu ulikamilishwa. Kwa hivyo, ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi katika suala hili. Kwa msingi wa uchambuzi, Mahakama iliona kwamba Maombi haya yalikidhi matakwa ya kukamilisha taratibu za ndani kuhusiana na kupinga vikawazo vinavyodaiwa kuwepo kwa mujibu wa sheria ya BRADEA.

Mahakama iliendelea kuangalia masharti mengine ya ukubalifu, na hatimaye ikaona kwamba Maombi haya yalikidhi matakwa mengine yote ya ukubalifu. Kwa hivyo Mahakama ilitangaza kuwa Maombi haya yanakubalika.

Hatimaye, Mahakama haikutoa uamuzi wake kuhusu uzingatiaji wa sheria, fidia na gharama za kushughulikia kesi.

**Kwa maelezo zaidi:**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na maelezo yote ya Hukumu ya Mahakama ya Afrika yanapatikana kwenye tovuti: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0412020

Kwa maswali mengine yote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni Mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kulinda Haki za Binadamu na Watu barani Afrika. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na hati nyingine yoyote ya Haki za Binadamu iliyoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org*